



PIGIA KITUO CHA SUMU

Vituo vya sumu vinaweza kutumiwa kwa mtu yeyote, sio watoto wadogo tu. Kwa hakika, **kuna mtu mpya anayetafuta huduma za kituo cha sumu kila sekunde 8.** Bahati nzuri ni kwamba, unaweza kupigia simu kituo cha sumu kwa haraka, bila malipo na kwa siri.



Okoa muda na pesa

Wataalamu wa sumu wanaweza kusaidia kutua matatizo mengi kuititia simu. Hii inaweza kukuokoa muda wa kutembelea daktari au hospitali.

Madaktari wa Matibabu hupigia kituo cha sumu, pia

Wahudumu wa afya hupigia kituo cha sumu kwa usaidizi wa kuwatibu wagonjwa wao waliopata sumu.



ACHA KUTAFUTA USAIDIZI KWENYE INTANETI. CHUKUA SIMU NA UPIGE.

USAIDIZI BILA MALIPO, WA HARAKA, WA KITAALAMU KWA SAA 24 KWA SIKU, SIKU ZOTE 7 ZA WIKI.

1-800-222-1222

Kituo cha Udhibiti wa Sumu (Poison Control Center) hutoa ushauri wa mara moja wa matibabu kwa dharura za sumu. Wafamasia, wauguzi na madaktari wanapatikana kwa saa 24 kila siku ili kutoa huduma kwa watu wa umri wowote. Huduma zote hazilipishwi na ni za siri, na usaidizi unapatikana katika lugha zaidi ya 150.



*Usaidizi usiolipishwa, wa haraka na wa kitaalam.
Saa 24 kwa siku. Siku zote 7 za wiki.*



Upstate New York Poison Center
www.upstatepoison.org


brosha iliyoundwa na:
Utah Poison Control Center
University of Utah Health
College of Pharmacy, L.S. Skaggs Pharmacy Institute

Swahili



Simu ya Dharura ya Kituo cha Sumu

Kituo cha Sumu cha Juu cha New York





FAHAMU HATARI

Karibu kila kitu kinaweza kuwa na sumu kikitumiwa vibaya, kwa kiasi kisichofaa au na mtu asiyefaa. Kutumia kiasi kisicho sahihi cha dawa au dawa ya mtu mwingine, kuchanganya visafishaji, au kunywa pombe kupita kiasi kunaweza kusababisha athari za sumu.

Sumu Zinazowezekana



Dawa (dawa za kuagizwa na daktari, dawa zisizo za kuagizwa, dawa za mitishamba)



Dawa zingine




Bidhaa za nyumbani za usafi wa binafsi, za usafishaji, utunzaji wa bustani na za matengenezo ya gari



Kuumwa na kuchomwa miiba



Uyoga na mimea



Moshi na gesi

VIDOKEZO VYA KUZUIA ATHARI ZA SUMU

Iwapo unafikiri mtu amepata athari za sumu, piga simu kwa **1-800-222-1222** mara moja. Mtu aliyejata athari za sumu wakati mwininge huwa haonyeshi dalili mara moja.

Hakikisha usalama nyumbani kwako

- Hifadhi nambari ya 1-800-222-1222 katika simu yako ya mkononi kama mwasiliani wako wa kudhibiti sumu. Bandika nambari kwenye friji au karibu na simu za nyumbani na ofisini endapo kutakuwa na dharura ya sumu.
- Weka dawa na bidhaa za nyumbani kwenye vyombo vyake asilia mbali na chakula.
- Soma kila mara lebo kwenye bidhaa au dawa na ufuate maelekezo kwa matumizi salama.
- Kuwa na kengele ya monoksidi ya kaboni nyumbani kwako. Badilisha betri mara kwa mara na uhakikishe kuwa zinafanya kazi vizuri.



Chunga watoto

- Weka bidhaa za nyumbani na dawa zikiwa zimefungiwa mahali ambapo watoto hawawezi kuziona au kuzifikia.
- Tumia vifungashio visivyoweza kufunguliwa na watoto. Lakini kumbuka, hakuna kitu chochote huwashinda watoto kabisa!
- Kamwe usiite dawa "pipi."
- Sumu zinaweza kuonekana kama chakula au kinywaji. Wafundishe watoto kumwuliza mtu mzima kabla ya kuonja chochote.
- Zungumza na watoto na vijana kuhusu hatari za kutumia dawa au bidhaa nyingine ili "kulewa" au kushiriki katika mchezo ya kuthubutu.

HUDUMA YA KWANZA KWA ATHARI ZA SUMU

Ikiwa mtu ataacha kupumua, atazimia au atapata kifafa, piga simu kwa **911** mara moja.

Kwa hali zote zifuatazo, pigia simu kituo cha sumu kilicho karibu kwa 1-800-222-1222.



Sumu machoni

Osha macho kwa maji ya mfereji na upigie simu kituo cha sumu.



Sumu kwenye ngozi

Vua mavazi yoyote ambayo yameguswa na sumu. Osha ngozi kwa maji ya mfereji na upigie simu kituo cha sumu.



Sumu ya kuvuta hewa ndani

Nenda katika eneo lenye hewa safi mara moja na upigie simu kituo cha sumu.



Sumu iliyomezwa

Usijaribu kutumia tiba za nyumbani au kujaribu kumfanya mtu atapike. Pigia simu kituo cha sumu kilicho karibu kwanza.

PIGA SIMU 1-800-222-1222 KWA DHARURA YA SUMU NA MASWALI YA SUMU